

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI



16 APRILI, 2018

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA KUMI – TAREHE 16 APRILI, 2018

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS
(MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019).

III. MASWALI:



OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**77. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR
(NYANG’HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kwa juhudi zake Mbunge wa Jimbo la Nyang’hwale ameanzisha ujenzi wa

baadhi ya majengo ya Zahanati kubwa na za kisasa katika Vijiji vya Nyamikonze na Iyenze:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kusaidia kukamilisha ujenzi huo;

(b) Je, Serikali ipo tayari kuifungua Zahanati iliyojengwa na Mbunge katika Kijiji cha Mwamakilinga ambayo imekamilika tangu Novemba, 2014.

78. MHESHIMIWA HAMIDU HASSAN BOBALI (MCHINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali imefanya tathmini juu ya ubora na changamoto zilizopo katika Shule za Sekondari za Kata nchini.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

79. MHESHIMIWA JOHN JOHN MNYIKA (KIBAMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ujenzi wa barabara za mzunguko/mchepuko kwa kiwango cha lami ni

muhimu katika kupunguza msongamano kwenye barabara kuu ya Morogoro:-

(a) Je, ni lini barabara ya Tangibovu – Kibaoni – Goba – Mbezi - Malamba Mawili - Kinyerezi utakamilika;

(b) Je, ni lini ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara zingine za mzunguko/mchepuko katika Jimbo la Kibamba utaanza.

80. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha za kujenga barabara ya Tendo – Muze (km 37.04) kwa kiwango cha lami.



WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:

81. MHESHIMIWA SIKUDHANI YASINI CHIKAMBO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, Serikali inaweza kueleza ni miradi ipi ya maji mikubwa na midogo iliyokamilika na isiyokamilika katika Mkoa wa Ruvuma na Wilaya zake zote.

**82. MHESHIMIWA VICTOR KILASILE
MWAMBALASWA (LUPA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bwawa la Matwiga Wilayani Chunya.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

**83. MHESHIMIWA DEVOTHA MATHEW MINJA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:- Wamiliki wa majengo wameanza kupangisha majengo kwa kutumia fedha za kigeni kama vile Dola ya Kimarekani badala ya fedha ya Kitanzania hali inayosababisha kuendelea kuporomoka kwa thamani ya Shilingi:-

Je, Serikali ina mpango gani kuchukua hatua kulinda thamani ya Shilingi.

**84. MHESHIMIWA GODFREY WILLIAM MGIMWA
(KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni nini tamko la Serikali juu ya idadi kubwa ya Benki za kibiashara kufunguliwa kwenye Miji mikubwa tu.

WIZARA YA NISHATI:

**85. MHESHIMIWA RIDHIWANI JAKAYA KIKWETE
(CHALINZE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:- Maeneo mengi ya Halmashauri ya Chalinze yamefaidika na mradi wa REA Awamu ya II, lakini katika utekelezaji wa mradi huo Miji ya Kiwangwa, Hondogo, Mkange na Kibindu bado haijafikiwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuifikia Miji hiyo.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

86. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (BLW):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:- Kwa muda mrefu sasa Kurugenzi nyingi za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki zimekuwa zikiongozwa na Makaimu hali ambayo inapunguza ufanisi wa kazi:-

Je, ni sababu gani za msingi zinazoifanya Serikali kushindwa kuwathibitisha Makaimu hao.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI) NA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
16 APRILI, 2018**

**S. KAGAIGAI
KATIBU WA BUNGE**